

# SEHEMU ZA KUPATA HABARI

## Sehemu ya kwanza 1 Maelezo ya awali ya takataka

### Nini taka?

Kitu chochote kilichotumika na kutupwa baada ya matumizi huitwa takataka. Katika Kiswahili neno taka au uchafu pia hutumika kwa maana sawa na takataka! Zaidi ya watu billion 7 hivi sasa wanaishi katika sayari yetu na kila mmoja anazalisha takataka baada ya matumizi mahitaji yao. Takataka zinaweza kuwa karatasi, mabaki ya chakula, vibati, vigae, plastiki na miswaki mikongwe... kitu chochote tunachotupa!!!



*Tafuta takataka zinatoka wapi katika Zanzibar -fikiria kuhusu nyumbani kwako, skuli, pahala pa kazi na jamii.*

### Aina za takataka

**Taka zinazooza:** Kimaumbile takataka zinaweza kuharibika au kuoza zinapokumbana na wadudu wadogo kama bakteria. Mfano karatasi, mbogamboga na maganda ya matunda, mabaki y chakula na takataka za bustani. **Taka zisizooza:** haziharibiki au zinachukua miaka mingi kuharibika. Mfano plastiki, jamii ya chuma na gilasi.



Je! Wewe unaoza? Ndio, binadamu ni sehemu ya maumbile asilia ambapo maumbile asilia huwa na njia za kushughulikia miili ya viumbe waliofariki: vijidudu-ardhi humong'onyoa, virutubisho na maadini husarifiwa tena upya.

Takataka zinazotishia mazingira ni zile zinazotoa sumu, zinazo babua (kuunguza), kuripuka au kutoa michanganyiko hatari ya kemikali. Takataka hizi huitwa taka za hatari kubwa (hazardous).



Taka hatarishi zinaweza kuwa katika hali ya ugumu, maji maji au katika umbile la gesi, na hutokana na vyanzio tofauti kutoka majumbani. (Mfano betri, rangi, mafuta ya gari kwenye kilimo kama dawa za kuulia wadudu au viwanda mfano chemikali).

### Tatizo: Takataka huenda wapi baada ya kutupwa?

Hapo zamani, vikundi vidogo vidogo vya wawindaji vilikuwa na maisha ya kawaida ya kutoka sehemu moja kwenda nyengine. Maumbile kwa hivyo yaliwawezesha kushuhulikia takataka zao. Watu walikula vyakula vyenye kuvunjwa vunjwa na bakteria kwa njia za kibaolojia, na zana za kufanyia kazi zilitengenezwa kwa kutumia mifupa au mawe. Watu walipoanza kuishi kama wakulima, waliendeleza zoezi la kuchoma taka taka kwa kuweka usafi wa nyumba zao na kujiepusha na wadudu. Katika mashamba yao uchomaji taka taka hurejesha virutubisho katika ardhi. Tokea yalipoanza mapinduzi ya viwanda tumeshatengeneza vitu vingi ambavyo haviwezi kusagika kwa nguvu za kimaumbile.

## Uzalishaji wa takataka katika ulimwengu wa leo unasababisha matatizo makubwa

### ① Takataka nyingi mno

Takataka zinazotupwa kila mahali. Watu hutupa takataka ardhini, bustanini na baharini. Je hii ni sahihi kufanya hivyo? Hapa na, sio sahihi!

*“Mtindo maisha wa kila mmoja wetu huzalisha kwa wastani wa kilo moja ya taka taka kwa siku!!! Ni kiasi gani WEWE huzalisha taka taka kwa siku?”*



② **Uchafuzi wa mazingira:** unahusisha vitu vingi vya hatari ambavyo hutupwa ardhini, katika maji, baharini hata angani ambapo vinaweza vikaharibu sayari yetu, wanadamu na siha za wanyama.

#### 2.1. Uchafuzi wa ardhi

Takataka nyingi zinazozalishwa majumbani au skuli aidha huchomwa au hutupwa katika maeneo yanayojulikana kuwa ni **mashimo ya takataka**. Shimo la takataka ni shimo ambalo huchimbwa ardhini na kujazwa takataka mpaka liwe halina nafasi tena. Takataka za maeneo ya mji mkongwe hupelekwa katika shimo limetengwa maalum kwa shughuli hiyo. Sehemu zilizobakia za Unguja zina majaa ya wazi ambayo huvutia panya na kunguru. Kemikali zenye madhara zinazotokana na rangi, betri na dawa za kuulia wadudu huingia ardhini, haviharibiki bali hujijenga katika viwiliwili vya miti, wanyama na wanadamu ambao hutumia miti hiyo kwa chakula. Hali hii inaathari kubwa kwa maumbile na afya zetu.



(© Zanrec)

#### 2.2. Uchafuzi wa maji

Maji yaliyochanganyika na takataka huitwa maji taka au maji machafu. Maji machafu mara nyingi huwa ni mikojo na vinyesi vya wanadamu ambavyo vina bacteria ambao husababisha maradhi kama kipindu pindu (cholera) au ugonjwa wa matumbo (typhoid). Zanzibar haina utaratibu wa kushuhulikia mitaro na kuiweka katika hali ya usalama. Watu wachache wanatumia vyoo vya mashimo na katika kadhia nyingi wengi wao huwa hawana uchaguzi wanalazimika kwenda misituni au kwenye fukwe. Mara kwa mara fukwe huchafuka kwa nepi chafu. LO!!!



(© fredhoogervorst.com)

#### 2.3. Uchafuzi wa bahari

Zanzibar imezungukwa na bahari ya Hindi. Haishangazi ikiwa mawimbi, upepo, maji kujaa na kupwa mara kwa mara huondosha uchafu katika fukwe.

Uzuri ulioje!! Lakini kweli zimetoweka kwa sababu hatuzioni tena popote pale?? HAPANA!!! Takataka zilizomalizikia baharini zina athari kubwa kwa viumbe vinavyoishi baharini kama vile samaki na matumbawe.

Wingi wa plastiki baharini unaweza kuwachanganya wanyama wanaotafuta chakula. Mfano kwa kasa, mfuko wa plastiki unaoelea hufanana na Jelly fish, na vipande vidogo vya plastiki baadhi



(© <http://www.amcs.org.au>)



# ENEO LA HABARI

ya wakati huonakana kama mayai ya samaki kwa ndege wa baharini. Makosa haya huweza kusababisha matatizo ya tumbo kwa viumbe hao na mwisho hufariki. Pia uvuvi wa nyavu mara kwa mara huvunja matumbawe na hupoteza maisha ya viumbe wa baharini kama vile pomboo na kasa au kobe (turtle).

## 2.4. Uchafuzi wa anga

Hewa inaharibika kupitia uchomaji takataka ambao ni zoezi maarufu kwa Zanzibar. Tunapochoma plastiki, mpira na betri tunapata moshi wenye sumu unao-weza kusababisha matatizo ya kiafya kama vile matatizo ya mapafu, ngozi na kuwashwa kwa macho.

## ③ Utumiaji wa mali asili

Nguvu nyingi na mali asili hutumika wakati uzalishaji na mwisho huishia takataka. **Mali asili** ni vitu ambavyo vinatolewa na ardhi mbayo tunavitumia na tunavitegemea kimaisha kama vile mbao, maji, mafuta na maadini. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu duniani, baadhi ya mali asili kama vile mafuta hazitomalizika milele.

(© Ulli Kloiber)

